

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO

Anuani ya Simu: "Kilimo Dodoma"

Nambari: +255 26 2321407

Fax: +255 26 2320037

Email: ps@kilimo.go.tz



Idara ya Utawala,
Mji wa Serikali - Mtumba,
S.L.P. 2182,
DODOMA.

**TAARIFA KWA UMMA KIKAO CHA WAZIRI WA KILIMO NA
MAAFISA KILIMO WA MIKOA NA HALMASHAURI**

Dodoma, 27 Januari 2021

Wizara ya Kilimo imeandaa kikao kazi cha Waziri wa Kilimo na Maafisa Kilimo wa Mikoa na Halmashauri nchini kwa lengo la kujadili changamoto za upatikanaji huduma za ugani na nini kifanyike kuwasaidia wakulima kuboresha kilimo ili kiwe na tija.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Waziri wa Kilimo Mhe. Prof. Adolf Mkenda (Mb) kikao hicho kitajadili na kuweka mikakati ya utekelezaji wa kuhakikisha Wizara inaleta mapinduzi makubwa na kukifanya kilimo kuwa cha kisasa na chenye faida kwa mkulima kwa kuzingatia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II).

Mkutano huo utafanyika **tarehe 29-30 Januari, 2021 katika ukumbi wa Mikutano wa LAPF Jijini Dodoma** kuanzia saa 3.00 asubuhi. Katika kikao hicho Wizara itaelezea vipaumbele na mwelekeo wake katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2020-2025).

Imetolewa na:

Handwritten signature of Gerald M. Kusaya in blue ink.

Gerald M. Kusaya

KATIBU MKUU